



NAETISL

National Association of
Educational Translators and
Interpreters of Spoken Languages



MODDC

Missouri
Developmental
Disabilities Council

Kuelewa Elimu Maalum: Muhtasari Kwa Wazazi

Funding for the Supporting Language Access in Schools Project in Missouri provided by the Missouri Developmental Disabilities Council, was supported by the Administration for Community Living (ACL), U.S. Department of Health and Human Services (HHS) as part of a financial assistance award totaling \$1,361,246 with 100 percent funding by ACL/HHS. The contents are those of the author(s) and do not necessarily represent the official views of, nor an endorsement, by ACL/HHS, or the U.S. Government.



naetisl@gmail.com

NAETISL



Follow us



MODDC



moddc@moddcouncil.org



www.naetisl.org

www.moddcouncil.org





Kuelewa Elimu Maalum: Muhtasari Kwa Wazazi

Elimu Maalum ni nini?

Elimu maalum ni maagizo yaliyoundwa mahususi ili kukidhi mahitaji ya kipekee ya mtoto mwenye ulemavu. Elimu hii huwasaidia wanafunzi kujifunza kwa njia inayowafaa zaidi, iwe katika madarasa ya elimu ya jumla, vikundi vidogo, au kupitia huduma zinazohusiana, kama vile hotuba au tiba ya kazi.

Nani anastahiki kupata Elimu Maalum?

Mtoto anaweza kupata iwapo

- Ako na ulemavu (kwa mfano, ulemavu wa kujifunza, usonji, ugonjwa wa upungufu wa tahadhari, kuongea/kuchelewa kuongea, uziwi)
- Anahitaji maelekezo maalumu kufaulu shuleni
- Ako kati ya miaka 3 hadi 22

Ustahiki hubainishwa kupitia mchakato wa tathmini na kuongozwa na sheria ya shirikisho chini ya Sheria ya Elimu ya Watu Wenye Ulemavu (IDEA).

Watoto wachanga walio na ucheleweshaji wa maendeleo ama ulemavu, tangu kuzaliwa hadi miaka 3, wanaweza kuhitimu kwa huduma hizi.

Nitajuaje kama mtoto wangu anahitaji Elimu Maalum?

Unaweza kumwona mtoto wako:

- Anapata changamoto katika kusoma, kuandika, ama hesabu
- Ana shida ya kuzingatia, kutukia, ama kukamilisha kazi zake
- Ana ugumu wa mawasiliano ama kuingiliana kijamii





- Hana maendeleo shuleni ingawa anapata usaidizi kutoka kwa mwalimu

Kama uko na wasiwasi, unaweza kuomba tathmini kupitia kwa shule ya mtoto wako.

Tathmini ni nini?

Tathmini ni seti ya kina ya majaribio na uchunguzi ambayo huangalia jinsi mtoto wako anavyojifunza, kutenda, na kuwasiliana. Inatumika kuelewa uwezo na changamoto za mtoto wako. Wataalamu waliohitimu pekee, kama vile mwanasaikolojia wa shule au mwalimu, husimamia majaribio haya.

Shule lazima ipokee idhini yako iliyoandikwa kabla ya kufanya majaribio hayo.

IEP ni nini?

Watoto wanaostahiki kupata elimu maalum hupokea Mpango wa Kibinafsi wa Kielimu (IEP). Mpango huo ni karatasi la kisheria ambalo:

- Hueleza mahitaji ya kujifunza ya mtoto wako
- Linaorodhesha malengo ya mwaka
- Hutoa maelezo ya huduma na msaada ambao shule itapeana

Mpango wa IEP umeundwa na kundi linalokujumuisha wewe, waalimu, wataalamu, na nyakati zingine, mtoto wako.

Kama hautaki mtoto wako apokee huduma za elimu maalum au iwapo haukubaliani na ule mpango wa kibinafsi wa kielimu yaani IEP, unaweza kukataa kuidhinisha huduma hizo.





Je, mtoto wangu anaweza kupata huduma gani?

Kulingana na mahitaji yake, mtoto wako anaweza kupokea:

- Usaidizi wa ziada katika kusoma au hesabu
- Tiba ya kuongea au lugha
- Tiba ya kufanyisha kazi viungo vidogo vya mwili au tiba ya mwili
- Mafunzo ya ujuzi wa kijamii
- Mashauri au msaada wa tabia
- Usaidizi wa ziada (k.m., muda zaidi kwenye mitihani)

Je, mtoto wangu ataondolewa kutoka kwa darasa lake la jumla?

Sio lazima. Watoto wengi walio kwenye mafunzo ya IEP hutumia muda wote au mwingi katika madarasa ya elimu ya jumla kwa usaidizi wa ziada. Kundi la IEP huamua mazingira yenye vikwazo vya chini (LRE) ambayo ni sawa kwa mtoto wako.

Je, haki zangu kama mzazi ni gani?

Uko na haki ya :

- Kujihusisha na mikutano yote
- Kukagua na kuomba mabadiliko kwa IEP
- Kupokea ripoti ya maendeleo ya mtoto wako
- Kukataa maamuzi na kuomba upatanishi au kusikilizwa
- Kupata rekodi zote za masomo

Je, naweza kufanya nini kumsaidia mtoto wangu?

- Uliza maswali na fuatilia habari
- Hifadhi nakala zote za ripoti pamoja na IEP
- Endeleza mawasiliano na waalimu na watoa huduma
- Himiza kujifunza nyumbani kwa mazoea na kutia moyo
- Jiunge na vikundi vya wazazi karibu na wewe na mashirika ya utetezi





NAETISL



MODDC

Je, naweza kupata maelezo zaidi wapi?

Zungumza na mratibu wa elimu maalum wa shule yako au tembelea tovuti ya elimu maalum ya jimbo lako kwa nyenzo zaidi.

Nawezaje kupata usaidizi katika lugha yangu?

Omba huduma za mkalimani katika shule ya mtoto wako au katika ofisi za wilaya ya shule. Omba habari iliyotafsiriwa na kuandikwa ikiwa inahitajika. Taarifa zinazopatikana kwa wazazi wote katika wilaya ya shule zinapaswa kupatikana kwako pia.

 naetisl@gmail.com

 www.naetisl.org

NAETISL



Follow us 



MODDC



moddc@moddcouncil.org 

www.moddcouncil.org 